

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيُسْتَخْلَفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَإِنَّكُمْ لَمْ تَكُونُوا أَنْصَارَهُمْ وَلَيَسْبِدَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَهُمْ أَمَّا
يَعْمَدُونَ فِي لَا يُشْرِكُونَ بِإِيمَانِهِمْ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Taarifa kwa Vyombo nya Habari

[مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رَجُلٌ صَدَقَوَا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَنْ قَضَى نَحْبَهُ
وَمِنْهُمْ مَنْ يَنْتَظِرُ وَمَا بَدَأُوا تَبْدِيلًا]

**“Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu.
Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata
kidogo.” [Al-Ahzab: 23]
(Imetafsiriwa)**

Hizb ut Tahrir / Wilayah Lebanon inamuomboleza shahidi Ahmed Saleh Al-Ali, ambaye mauwaji yake yaliothibitika kufanya na mikono ya serikali ya kihalifu ya familia ya Assad nchini Syria, baada ya miaka mingi ya kukosekana kwake mnamo 1980 katika magereza ya dikteta aliyefariki Hafez al-Assad.

Shahidi huyu shujaa hakika alibeba ulinganizi wa kuregesha maisha kamili ya Kiislamu na kusimamisha Khilafah kwa Njia ya Utume ubebaji wa kweli, kuanzia Lebanon, hadi Uturuki, kisha Syria, akiwacha nyuma yake mapambo ya maisha ya dunia, akimuelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu, mpaka akawa miongoni mwa mabwana wa mashahidi, hivi ndivyo tunavyo muhisabu, na Mwenyezi Mungu anajua zaidi, kwa kusadikisha Hadith ya Mtume (saw):

«سَيِّدُ الشُّهَدَاءِ حَمْزَةُ بْنُ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ، وَرَجُلٌ قَامَ إِلَى إِمَامٍ جَانِبٍ فَأَمَرَهُ وَنَهَاهُ، فَقَتَلَهُ»

“Bwana wa mashahidi ni Hamza ibn Abdul Mattalib, na mtu anayesimama mbele ya mtawala jeuri akamuamrisha mema na kumkataza maovu kisha (mtawala huyo) akamuua (kwa sababu hiyo).”

Na sisi tunapomuomboleza leo baada ya kuthibitika shahada yake, mikononi mwa madhalimu, hakika damu ya Ahmed Saleh Al-Ali, na waliomtangulia na baada yake miongoni mwa ndugu zetu, katika da'wah hii nzuri na iliyobarikiwa, haitapotea bure kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na kesho iliyokaribu mno itasimama Dola ya Kiislamu, Khilafah kwa Njia ya Utume, na italipiza kisasi kikali kwa madikteta madhalimu, na itanyanya jina la Ahmed Saleh Al-Ali na ndugu zake, wanaume katika njia ya da'wah hii, na viigizo vyema vinavyoigwa katika subira na msimamo na kujitolea katika kuregesha maisha kamili ya Kiislamu na kusimamisha Khilafah kwa Njia ya Utume.

Mwenyezi Mungu akukubalie Ewe Abu Muhammad, na akupandishe katika Pepo ya 'I'Iyeen' pamoja na mitume na wakweli na mashahidi na watu wema na hao ndio marafiki wazuri, na waliosalia nyuma katika ndugu zako miongoni mwa wabebaji da'wah, na wanaofuata nyayo zako, ni watu wema, wanaobeba bendera ('Iwa'a) ya ulinganizi kwa subira na msimamo na uume.

[وَاللهُ غَالِبٌ عَلَىٰ أَمْرِهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ]

“Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kushinda katika jambo lake, lakini watu wengi hawajui.”[Yusuf: 21]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Lebanon**